JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA WAZIRI MKUU
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA GEITA

**MKOA WA GEITA:** S.L.P. 139,
**GEITA**

Tafadhali unapojibu taja:
**Kumb. Na. LA./229/306/01/15**

**22/02/2026**

MTENDAJI MKUU,
TUME YA MADINI,
S.L.P 2292,
**DODOMA.**

**YAH: UKAGUZI WA MAZINGIRA WA MRADI WA UCHENJUAJI WA MAWE/MCHANGA WA DHAHABU KATIKA KIJIJI CHA SOBORA, KATA YA MAGENGE, HALMASHAURI YA WILAYA YA GEITA**

Tafadhali husika na somo tajwa hapo juu.

2. Idara ya Mazingira ilifanya ukaguzi wa Mazingira tarehe 20/02/2026 katika eneo la Kampuni ya **NANJIRINJI'S MINERALS COMPANY LIMITED** inayotarajia kufanya shughuli za uchenjuaji wa mawe/mchanga wa dhahabu katika kijiji cha Sobora, Kata ya Magenge, Halmashauri ya Wilaya ya Geita.

3. Shughuli ya ukaguzi ilifanyika kutokana na utaratibu wa kwamba kabla mradi kuanza au mradi ukiwa unaendelea kufanya kazi lazima ukaguzi wa kitaalam kuhusu masuala ya Mazingira ufanyike katika eneo la mradi husika. Mwekezaji aliomba Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya ya Geita kukagua eneo la mradi na kutoa ushauri. Ukaguzi huo ulifanywa na kamati ya Mazingira ya kijiji na Idara ya Mazingira Halmashauri ya Wilaya ya Geita.

3. Taarifa ya ukaguzi imeambatishwa kwenye ukurasa unaofuata.

Nawasilisha;

Isack Abed
**Kny: Mkurugenzi Mtendaji (W)**
**GEITA**

K.n.y MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA GEITA

**Barua pepe:** ***ded@geitadc.go.tz*, Simu Na.: *028-25200610*, Nukushi Na.: *028-2520003***

Scanned with CamScanner

**Nakala:-**

Kamishna wa Madini,
Barabara ya Kikuyu,
S.L.P 422
**DODOMA**

Afisa Madini Mkazi –Kwa Taarifa
S.L.P 26
**GEITA**

Mkemia Mkuu - Kanda ya ziwa
S.L.P 502,
**MWANZA**

Scanned with CamScanner

# TAARIFA YA UKAGUZI WA MAZINGIRA WA MRADI WA UCHENJUAJI WA MAWE/MCHANGA WA DHAHABU KATIKA KIJIJI CHA SOBORA, KATA YA MAGENGE, HALMASHAURI YA WILAYA YA GEITA

## 1.0 UTANGULIZI.

**NANJIRINJI'S MINERALS COMPANY LIMITED** ni Kampuni ya uwekezaji iliyosajiliwa na wakala wa usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) na kupewa nambari ya usajili **189878702** ya tarehe 07/10/2025. Kampuni hii inatarajia kujishughulisha na shughuli za uchenjuaji (Ukamuaji) wa dhahabu kutokana na mawe/mchanga wa dhahabu kwa kutumia njia ya Carbon in Leach (C.I.L plant). Eneo la mradi lipo umbali wa kilomita 15.8 kutoka mamlaka ya mji mdogo wa Katoro na linafikika kwa barabara ya Katoro – Ushirombo.

## 2.0 UKAGUZI WA ENEO LA MRADI:

Kutokana na utaratibu wa kwamba kabla mradi kuanza au mradi ukiwa unaendelea kufanya kazi lazima ukaguzi wa kitaalam kuhusu masuala ya Mazingira ufanyike katika eneo la mradi husika. Wawekezaji waliiomba Ofisi ya Mazingira Wilaya ya Geita kukagua eneo la mradi na kutoa ushauri. Ukaguzi huo ulifanywa na kamati ya Mazingira ya kijiji na Idara ya Mazingira Halmashauri ya Wilaya ya Geita.

Hivyo malengo mahususi ya ukaguzi huu wa mazingira kwenye eneo la mradi yalikua ni kama yafuatayo;

- Kutambua athari zinazoweza kutokea kwa mazingira na jamii kwa ujumla (Environmental and social impacts identification).
- Kukusanya taarifa za awali kuhusu hali ya mazingira (Baseline data collection).
- Kuhakikisha mradi unafuata sheria na kanuni za mazingira.
- Kutathimini usimamizi wa taka ngumu na majitaka.

Scanned with CamScanner

- Kutoa ushauri wa kitaalam kuhusu namna bora ya kupunguza athari za mazingira na jamii zinazoweza kutokana na mradi (Mitigation Measures).

Ukaguzi unaonesha kwamba;

i. Eneo la mradi ni tambalale na limezungukwa na vichaka,nyasi pamoja na miti.

ii. Eneo la Mradi lina ukubwa wa Ekari 17.

iii. Hakuna njia za maji za asili (natural drainage) kwenye eneo la mradi.

iv. Hakuna wanyama wa asili kwenye eneo la mradi.

v. Eneo la mradi lipo mbali na makazi ya watu takriban mita 600.

vi. Eneo la mradi haliingiliani na barabara kuu au barabara za vijiji na makazi ya watu.

vii. Eneo la mradi lipo mbali na vyanzo vya maji takribani kilometa 1.5

viii. Katika eneo hilo kuna shughuli za uchenjuaji wa madini ya dhahabu zinaendelea.

Kulingana na maelezo ya mtaalam wa mradi na mpangilio wa eneo la mradi (Layout plan) hakuna uchafuzi wowote wa Mazingira ambao unaweza kusababishwa na shughuli za mradi wenyewe. Hii ni kwa sababu zifuatazo:

- Wamiliki wa mradi walimpata Mtaalam Mwelekezi wa Mazingira (Registered Environmental Expert) Ndugu Cosmas Judas mwenye namba ya usajili NEMC/EIA/0007/2019. Mtaalam huyu ameshasajili mradi NEMC na mchakato wa kufanya Tathimini ya athari ya Mazingira na jamii (EIA) unaendelea ili kubaini athari zinazoweza kutokea na kuweka mikakati ya kukabiliana nayo.

- Ndani ya eneo la mradi patachimbwa bwawa la tope sumu (tailing storage facility) kwa ajili ya kuhifadhi tope na maji yenye sumu.

Scanned with CamScanner

- Eneo la mradi litajengewa uzio ili kuzuia mifugo, wanyama au watu kuingia eneo la mradi bila utaratibu.
- Eneo la uzalishaji litazungushiwa mfereji ambao utakusanya maji yote yanayotokana na mvua na kuyasafirisha mpaka kwenye tenki ambapo yatatumika kwa shughuli za uzalishaji.
- Maji yote yatakayochanganywa na dawa yatakuwa katika mzunguko na hakuna jinsi yeyote ya maji hayo kutoka nje ya eneo la mradi kwa sababu maji yakitoka nje yatatoka na dhahabu na kusababishia wamiliki wa mradi hasara.
- Mradi huu hautakuwa na aina yoyote ya mashine za kelele zitakazowafikia na kuwasumbua wananchi ukizingatia kwamba aina ya mradi huu hautakuwa na mitambo mikubwa itakayoweza kusababisha kelele.
- Makapi ya marudio yatakayopatikana baada ya uchenjuaji wa dhahabu yatatunzwa vizuri na hayatakuwa na dawa yeyote.
- Mchanga utakaokusanywa kwa ajili ya kuchenjua dhahabu na makapi/matope yake utatunzwa/utawekwa katika eneo ambalo litazungushiwa uzio ili kuzuia mchanga usitiririke nje ya eneo la mradi.

ix. Mradi ukiisha wahusika wa mradi watafanya uchunguzi wa kimaabara na kama mabaki yatakuwa na kemikali yatatibiwa kabla ya kuyarudisha kwenye Ardhi ili yasiharibu Mazingira, watafukia mashimo, miti na nyasi zitapandwa ili kurudishia uoto wa asili.

Scanned with CamScanner

## 3.0 MIUNDOMBINU TARAJIWA YA MRADI

Ifuatayo ni miundombinu inayotarajiwa kujengwa kwenye eneo la mradi;

a) Bwawa la tope sumu kwa ajili ya kuhifadhi maji na matope yenye sumu kutoka kwenye C.I.L

b) Mtambo wa kuchakata dhahabu kwa njia ya kuyeyusha na kukamata dhahabu kwa kutumia kemikali ya Sodium cyanide na kaboni (C.I.L).

c) Mashine tatu (03) kubwa za kusagia mawe ya dhahabu (Crusher).

d) Matanki sita (06) ya uchenjuaji wa dhahabu kwa kutumia kemikali ili kutoa dhahabu (Leaching tanks).

e) Jengo maalum la kuchomea dhahabu (Elution Plant).

f) Jengo moja (01) la Utawala lenye ofisi sita na vyoo vi nne.

g) Vyoo vinane (08) vilivyojengwa kwa kutenga jinsia (Me&Ke) pamoja na mabafu matatu (03).

h) Ofisi moja (01) ya mlinzi yenye choo kimoja na bafu moja.

i) Jiko moja (01) la kupikia lenye sehemu ya kulia.

j) Stoo mbili (02) kwa ajili ya kuhifadhia vifaa mbalimbali vitakavyokua vikitumiwa ndani ya eneo la mradi.

k) Gereji moja ya kutengenezea magari na mitambo mbalimbali itakayotumiwa na Kampuni.

l) Jengo moja la maabara lenye stoo kwa ajili ya kutunzia kemikali.

m) Transfoma moja kwa ajili ya kusambaza umeme kwenye maeneo mbalimbali ya mradi.

Scanned with CamScanner

n) Jenereta moja ambalo litatumika endapo umeme utakatika kwenye eneo la mradi. Jenerata hili litakua na uwezo wa kuzalisha umeme wa 700 KVA.

o) Ndani ya eneo la mradi patachimbwa visima vitatu (03) virefu vya Maji.

Scanned with CamScanner

## 4.0 MAPENDEKEZO:

i. Wawekezaji wa mradi wasajili mradi NEMC na wafanye Tathimini ya Athari ya Mazingira na jamii ili kubaini athari zinazoweza kutokea na kuweka mikakati ya kukabiliana nayo.

i. Wamiliki wa mradi wafike kwenye ofisi ya Mkemia Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kupata kibali cha kutumia kemikali na kupata maelezo zaidi juu ya kuhifadhi kemikali aina ya Cyanide ili kutoleta madhara kwa binadamu.

ii. Kwa kua mradi unahusisha miundombinu ya CIL wahusika wazingatie kupata kibali cha kutumia bwawa la tope sumu.

iii. Tunapendekeza wamiliki waendelee kutunza eneo la mradi kwa kupanda miti kuzunguka eneo la mradi na kutunza miti ya asili iliyopo.

iv. Wamiliki wa mradi wahakikishe maji yanayotumika kwenye shughuli za mradi hayatoki nje ya eneo la mradi kama mpangilio wa eneo la mradi unavyoonesha.

v. Wamiliki wa mradi wahakikishe wamechimba mfereji mrefu kuzunguka eneo la mradi na kuujengelea kwa saruji ili kuzuia maji yatakayotiririka wakati wa msimu wa mvua yasiende nje ya eneo la mradi au watengeneze tuta kubwa kwa kutumia udongo usio na sumu (kemikali) ili kukinga maji yanayotiririka wakati mvua zinanyesha yasiende nje na eneo la mradi.

vi. Wamiliki wa mradi wahakikishe watumishi wanavaa mavazi ya kuwakinga/kuzuia kugusa kemikali kama vile Glooves, buti, makoti, pamoja na mambo yote yanayoleta usalama kwa afya za wafanyakazi.

vii. Wamiliki wa mradi wahakikishe wanatenga eneo maalum kwa ajili ya kutunza kemikali, Chupa zote zenye kemikali zihifadhiwe vizuri na zifunikwe kwa uangalifu.

viii. Wamiliki wa mradi wahakikishe kuna vifaa vya msaada wa kwanza, iwapo kutatokea madhara ya kimwili kwa binadamu waweze kumhudumia mgonjwa kabla ya kupelekwa hospitali.

ix. Wamiliki wa mradi wahakikishe wanaweka vifaa vya kupambana na majanga ya moto (Fire Fighting equipments).

Scanned with CamScanner

x. Wamiliki wa mradi wahakikishe wanafuatilia ubora wa maji mara kwa mara (Regular water quality monitoring through monitoring bore holes).

xi. Kiongozi wa mradi ahakikishe ukaguzi wa Mazingira wa mara kwa mara unafanyika kwenye bwawa la tope sumu na Miundombinu mingine iliyopo ndani ya mradi.

xii. Wamiliki wa mradi wahakikishe wanaweka alama za usalama kwenye maeneo yote hatarishi yaliyopo kwenye eneo la mradi ili kuwalinda wafanyakazi kutokana na hatari mfano;No entry,no smoking,Fire exit,Emergency assembly point n.k.

xiii. Wamiliki wa mradi wahakikishe kwamba kuna mawasiliano (mahusiano) endelevu na jamii inayozunguka eneo la mradi.

Scanned with CamScanner

## 5.0 HITIMISHO:

Kutokana na ukaguzi uliofanyika katika eneo la mradi (ndani na nje) tumeridhika kwamba mradi huu hautaleta madhara ya aina yoyote katika Mazingira husika iwapo wamiliki wa mradi huu watafuata maelekezo kutoka kwa wataalam. Aidha, kama watakiuka maelekezo hayo baada ya kupewa kibali na kuanza kuendesha shughuli zao za uzalishaji, mradi huo utasimamishwa mpaka wamiliki wa mradi watakapokuwa wamefuata maelekezo ya kutunza Mazingira. Hivyo naomba wapatiwe kibali cha kuendesha shughuli hii kulingana na utaratibu uliopo. Eneo la mradi lipo kwenye coordinates zifuatazo:-

| CORNER | Latitudes | Longitudes |
|---|---|---|
| A | 03$^0$.117614S | 031$^0$. 952365E |
| B | 03$^0$.118707S | 031$^0$. 952128E |
| C | 03$^0$.117795S | 031$^0$. 950296E |
| D | 03$^0$.116854S | 031$^0$. 950371E |
| E | 03$^0$.114888S | 031$^0$. 950328E |
| F | 03$^0$.115049S | 031$^0$. 951289E |
| G | 03$^0$.116923S | 031$^0$. 951366E |

Scanned with CamScanner

Note:

- Wawekezaji watakapoanza shughuli za mradi wahakikishe wanalipa Kodi ya Huduma (Service levy) kwa Halmashauri husika pamoja na CSR

- Vifungashio vya sumu havitakiwi kutoka nje ya eneo lao la kazi bila kibali na watatakiwa kufuata maelekezo kutoka ofisi ya Mkemia Mkuu.

- Iwapo kutatokea ajali na vifo vinavyotokana na shughuli za mradi, mradi utasimamishwa bila kujali kibali kilichotolewa.

- Wawekezaji kabla hawajaanza kuzalisha wachimbe mitalo kuzunguka eneo lote kwenye uwelekeo wa maji na mitalo hiyo ijengelewe vizuri kuzuia maji ya sumu yasitoke nje ya eneo la mradi.

- Wawekezaji wachimbe mashimo na kuyajengelea kwa saruji na kumwaga zege kwa chini ili maji yote yakusanywe, pasiwepo na maji yoyote yanayotiririka kutoka kwenye eneo la mradi.

Scanned with CamScanner